

**Swali:** Tukisoma *Mwanzo 2:23*, tunaona Mwanamke Hawa pekee ndiye aliyetajwa kama “*Nyama na mfupa wa Adamu*” kwasababu alitwaliwa kutoka kwa Adamu..lakini tukiruka mpaka kwenye kitabu hicho hicho cha *Mwanzo 29:14*, tunaona Labani anamtaja Yakobo kama “*Nyama yake na mfupa wake*”. Sasa swali Yakobo atakuwaje nyama na damu ya Labani, ukilinganisha na kauli hiyo ya Adamu aliyomwambia Hawa?

Jibu: Tusome mistari hiyo..

*Mwanzo 2:22 “na ule ubavu alioutwaa katika Adamu Bwana Mungu akaufanya mwanamke, akamleta kwa Adamu.*

*23 Adamu akasema, Sasa huyu ni MFUPA KATIKA MIFUPA YANGU, NA NYAMA KATIKA NYAMA YANGU, basi ataitwa mwanamke, kwa maana ametwaliwa katika mwanamume”*

Turejee tena..*Mwanzo 29:12-14*

*Mwanzo 29:12 “Yakobo akamwarifu Raheli ya kuwa yeye ni NDUGU WA BABAYE, na ya kuwa ni mwana wa Rebeka. Basi akapiga mbio akampasha babaye habari.*

*13 Ikawa Labani aliposikia habari za Yakobo, mwana wa nduguye, akaenda mbio amlaki, akamkumbatia, akambusu, akamleta nyumbani kwake. Naye akamwambia Labani maneno hayo yote.*

*14 Labani akamwambia, Ndiwe kweli MFUPA WANGU NA NYAMA YANGU. Naye akakaa kwake muda wa mwezi mmoja”.*

Kauli ya **“Mfupa na Nyama”**, haipo tu kufunua au kuwakilisha mahusiano ya mke na mume, bali pia mahusiano ya kindugu.

Watu waliozaliwa familia moja, hao ni watu wenye *mfupa mmoja na nyama moja*, hata vipimo vya kibinadamu (vya kibaolojia) vinathibitisha hilo. Sasa Hawa alitwaliwa kutoka katika ubavu wa Adamu hivyo ni lazima atakuwa tu uhusiano wa kibaolojia na Adamu, na tukirudi katika hiyo habari ya Labani na Yakobo, tunasoma walikuwa ni mtu na mjomba wake, hivyo walikuwa ni ndugu (*nyama moja na damu moja na mfupa mmoja*).

Kwahiyo kwa hitimisho ni kuwa kauli ya “nyama moja na mfupa mmoja”  
Haikutumika tu kwa Adamu na Hawa bali pia kwa watu wenye  
mahusiano ya kidamu, na inatumika mpaka leo, ni sawa tu na kauli ya  
Mungu aliyosema kuwa “alimwumba mtu kwa mfano wake na sura yake  
(Mwanzo 1:26-27)” haikumfunga kwamba itumiwe na yeye tu, kwani  
tunaona Adamu alipomzaa Sethi katika Mwanzo 5:3 alisema maneno  
yanayokaribia kufanana na hayo kuwa “aliziaa mwana kwa sura yake na  
mfano wake”. Hivyo hata sisi ni sura na mfano wa wazazi wetu, licha tu  
ya kuwa na sura na mfano wa Mungu.

Na watu wote waliookoka, ni wa **Damu moja na mfupa mmoja na  
nyama moja (mwili mmoja)** na Yesu Kristo.

*Wakolosai 3:15 “Na amani ya Kristo iamue mioyoni mwenu; ndiyo  
mliyoitiwa KATIKA MWILI MMOJA; tena iweni watu wa shukrani”.*

*Waefeso 4:4 “Mwili mmoja, na Roho mmoja, kama na mlivyoitwa  
katika tumaini moja la wito wenu.*

*5 Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja”*

Kwanini Labani aseme Yakobo ni Mfupa wake na nyama yake?(Mwanzo 29:14)

Na wote walio damu moja na Kristo ndio ndugu zake Kristo, na hao ndio watakaorithi pamoja naye, kwasababu agano la urithi siku zote lipo kwa watu wenye undugu wa kidamu.

Je umefanyika kuwa mrithi wa ahadi za Mungu?.. Kumbuka tunafanyika kuwa warithi kwa njia ya kumwamini Bwana Yesu Kristo na kubatizwa kwa maji na kwa Roho Mtakatifu.

Bwana akubariki.

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Pia Kwa maombezi/ Ushauri/ Maswali/ Whatsapp:

Tuandikie katika BOXI la Maoni hapo chini au

Piga namba hizi: +255693036618 au +255789001312

**Mada Nyinginezo:**

**HAPANA MFUPA WAKE UTAKAOVUNJWA.**

**Kwanini Raheli aliiba miungu ya Baba yake, (Labani) Mwanzo  
31:19.**

Kwanini Labani aseme Yakobo ni Mfupa wake na nyama  
yake?(Mwanzo 29:14)

## **MWILI NA DAMU YA YESU KRISTO.**

**Kula uzao wa tumbo lako maana yake nini? (Kumbukumbu 28:53)**

## **JE UMEKUFA PAMOJA NA NANI?**

### **Rudi nyumbani**

Share on:  
WhatsApp